Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara kuhusu EBT ya Shule kutokana na Janga (P-EBT)
-na-
P-EBT ya Msimu wa Kiangazi kwa Watoto wa Shule (**Mpya!)

Mwaka wa Masomo wa 2020-2021 (*Tarehe 3 Juni 2021)*

Swali la 1: P-EBT ni nini?

Jibu: Ni msaada wa vyakula wa muda ulioidhinishwa na serikali ya shirikisho ili kusaidia kaya zilizoathirika na kufungwa kwa shule kutokana na COVID-19.

Swali la 2: Nani anastahiki msaada wa P-EBT?

Jibu: Kaya za Vermont zilizo na wanafunzi ambao kwa kawaida wangepokea milo isiyolipiwa au iliyopunguzwa bei shuleni chini ya Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana (National School Lunch Program). Msaada unapatikana kwa mwezi mmoja ikiwa mwanafunzi alitumia muda mwingi katika mwezi huo akisoma kupitia aidha muundo wa kujifunza kwa mbali au mseto.

Swali la 3. Ninawezaje kujua iwapo kaya yangu inastahiki?

Jibu: Shule ya mwanafunzi wako itaamua ikiwa mwanafunzi wako anastahiki, kulingana na vigezo vilivyotolewa na jimbo. Shule inaweza kuwasiliana nawe ili kuhakikisha kuwa wana taarifa sahihi kwenye faili. Tafadhali jibu ombi lao. Ikiwa unastahiki, utapata barua kutoka DCF inayoelezea jinsi na lini utapata msaada.

Swali la 4: Ikiwa tunastahiki, je, tutapokea vipi misaada hii?

Jibu: Ikiwa unapokea 3SquaresVT kupitia kadi ya EBT, utawekewa msaada wa P-EBT kwenye kadi hiyo. Ama sivyo, utapokea kadi maalum ya P-EBT. Ikiwa tayari umepokea kadi ya P-EBT kwa mwaka wa masomo wa 2020-2021, tafadhali tunza kadi hii kwani msaada wako utawekwa kwenye kadi hii. Tafadhali kumbuka kuwa sheria ya shirikisho ya *Families First Coronavirus Response Act* iliidhinisha shule ya mwanafunzi wako kushirikisha data inayohitajika na Idara ya Watoto na Familia (DCF) kwa madhumuni haya.

Swali la 5: Nilipokea kadi ya P-EBT msimu uliopita wa kuchipua (2020), lakini sina tena. Je, hilo litakuwa tatizo?

Jibu: Hapana. Kadi mpya zinatolewa kwa mwaka wa masomo wa 2020-20201. Ikiwa utapata msaada wako kwenye kadi maalum ya P-EBT, tafadhali tunza kadi mpya unayopata. Misaada ya ziada inaweza kuwekwa kwenye kadi hii kwa kuwa kuna zaidi ya duru moja ya malipo katika mwaka huu wa masomo.

Swali la 6: Nilipokea kadi yangu mpya ya P-EBT, lakini nikaipoteza, nikaitupa, iliibiwa au iliharibika. Je, inabidi nifanye nini?

Jibu: Tafadhali piga simu ESD ili uzungumze na mtaalam wa P-EBT kupitia 1-800-479-6151 chagua 7 ili upokee kadi nyingine.

Swali la 7: Je, misaada itatolewa lini?

Jibu: Duru ya kwanza ya misaada (kwa Septemba 2020 - Februari 2021) ilitolewa mnamo Aprili 2021. Misaada kwa Machi - Juni 2021 inatarajiwa kutolewa mnamo Julai 2021. Tarehe hizi zinaweza kubadilika, tafadhali endelea kutembelea tovuti hii kwa Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara yaliyosasishwa.

Swali la 8: Je, msaada wa P-EBT ni kiasi gani?

Jibu: Msaada unategemea muundo wa masomo ya mwanafunzi wako katika mwezi husika:

- $119.35 kwa mwezi wa masomo ya muundo wa mbali.
- Sehemu ya msaada kwa mwezi wa masomo ya muundo mahuluti (siku kadhaa shuleni, siku kadhaa kwa mbali). *Sehemu ya msaada kwa Septemba hadi Februari 2021 ulikuwa $71.61 kwa mwezi. Sehemu ya msaada kwa Machi – Juni ni mdogo kwa sababu ya shule kurudi zaidi kwa masomo ya muundo wa ana kwa ana katika msimu wa kuchipua:*
    - Machi $38.19
    - Aprili $37.51
    - Mei $$33.42
    - Juni $30.69
- Hakuna msaada unaotolewa kwa mwezi wa masomo ya ana kwa ana.

Swali la 9: Je, msaada wa P-EBT unalingana bila kujali idadi ya watoto katika kaya?

Jibu: Hapana. Msaada unakokotolewa kulingana na muundo wa mafunzo wa kila mwanafunzi na ustahiki kwa milo isiyolipiwa na iliyopunguzwa bei. Msaada unaweza kutofautiana kutoka mwanafunzi mmoja hadi mwingine.

Swali la 10: Ulezi wa mwanafunzi wangu umegawanyika kati ya kaya mbili. Nani atapata msaada?

Jibu: Msaada huo utatumwa kwa mtu mzima ambaye ameorodheshwa kama Mkuu wa Kaya na shule ya mwanafunzi. Huyu anaweza kuwa mtu mzima aliyewasilisha ombi la milo isiyolipiwa au iliyopunguzwa bei kwa ajili ya mwanafunzi, au mtu mzima aliyeorodheshwa kama mtu wa msingi wa mawasiliano katika mfumo wa shule. Shule ziliwasiliana na kaya mnamo Februari ili kuthibitisha ni nani anayepaswa kuorodheshwa kama Mkuu wa Kaya. Tafadhali wasiliana na shule ikiwa Mkuu wa Kaya anahitaji kusasishwa.

Swali la 11: Ninaweza kununulia nini msaada huu?

Jibu: Angalia orodha ya vyakula vinavyostahiki kwenye tovuti ya USDA.

Swali la 12: Ninaweza kutumia wapi kadi yangu ya P-EBT?

Jibu: Unaweza kuitumia kununua vyakula katika eneo lolote ambalo linakubali 3SquaresVT. Hii ni pamoja na maduka ya vyakula, maduka makubwa, maduka ya karibu, na masoko mengi ya wakulima katika Vermont. Pata maelezo zaidi kwenye ukurasa wa wavuti wa EBT .

Swali la 13: Sina watoto shuleni. Je, naweza kupata msaada huu?

Jibu: Hapana. Msaada huu ni kwa kaya tu ambazo watoto wao kawaida hupata chakula kisicholipiwa au kilichopunguzwa bei shuleni kupitia Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana na sasa wanahitaji kula milo hiyo nyumbani kwa sababu wanajifunza kwa muundo wa mbali au mseto.

Swali la 14: Je, msaada huu ni kwa watoto walio katika shule ya umma pekee?

Jibu: Hapana. Baadhi ya shule binafsi hushiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana, na watoto katika shule hizo wanaweza kustahiki msaada huu. Hata hivyo, shule nyingi binafsi hazishiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana, na wanafunzi wao hawastahiki msaada huu.

Swali la 15: Je, vipi kuhusu shule ambazo hutoa kifungua kinywa na chakula cha mchana bila malipo kwa wanafunzi wote wanaotumia Community Eligibility Provision (CEP) au Provision 2?

Jibu: Wanafunzi wote katika shule hizi watapata msaada wa P-EBT kwa miezi ambayo wanasoma katika muundo wa mafunzo ya mbali au mseto. Unaweza kuona orodha ya shule hizi kwenye tovuti ya AOE.

Swali la 16: Kila mtu katika shule ya mtoto wangu kawaida hupata kifungua kinywa kisicholipiwa kupitia Provision 2. Je, kila mtu atapata msaada wa P-EBT?

Jibu: Hapana. Msaada unapatikana tu kwa wanafunzi katika shule ambazo kwa kawaida hutoa kifungua kinywa na chakula cha mchana bila malipo kupitia Provision 2 au CEP. Ikiwa shule yako kwa kawaida hutoa kifungua kinywa kisicholipiwa kwa kutumia Provision 2, ustahiki wa P-EBT utategemea ustahiki wa kila mwanafunzi kwa chakula cha mchana kisicholipiwa na kilichopunguzwa bei.

Swali la 17: Shule yetu inatoa milo isiyolipiwa kwa watoto wote mwaka huu. Je, hiyo inamaanisha wanafunzi wote watapata msaada?

Jibu: Hapana. Ikiwa shule ya mwanafunzi wako kwa kawaida haitoi "Milo kwa Wote" kupitia CEP au Provision 2 basi ustahiki utategemea ustahiki binafsi wa mwanafunzi kwa milo isiyolipiwa au iliyopunguzwa bei. Shule zinaweza kutoa milo isiyolipiwa kwa watoto wote mwaka huu kwa kutumia Mpango wa Huduma ya Vyakula wa Msimu wa Kiangazi wa USDA (Summer Food Service Program), lakini hiyo haitafanya wanafunzi wote shuleni wastahiki P-EBT.

Swali la 18: Mtoto wangu anafundishwa nyumbani mwaka huu. Je, tunastahiki msaada huo?

Jibu: Hapana. Msaada wa P-EBT unapatikana tu kwa wanafunzi ambao wameandikishwa katika shule ambayo kawaida hushiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana. Msaada unapatikana kwa wanafunzi waliojiandikisha ambao wanajifunza kwa mbali, lakini sio kwa wanafunzi ambao wamejiondoa kutoka shule yao na kufanya mafunzo ya nyumbani kwa mwaka huu. Wanafunzi wanaofanya mafunzo ya nyumbani wanaweza bado kupokea milo kutoka kwenye maeneo ya milo inayotolewa kwa watu wote. Tembelea Tovuti ya Kutafuta Milo ya USDA ili upate eneo la milo inayotolewa kwa watu wote karibu nawe.

Swali la 19: Nimekuwa nikichukua chakula cha mchana kwa ajili ya mtoto wangu katika eneo la *Kuchukua na Kuondoka* la shule yetu au wamekuwa wakituletea. Je, napaswa kusitisha kufanya hivyo ikiwa nitapokea msaada wa P-EBT? Je, itafanya tusistahiki msaada?

Jibu: Hapana. Wanafunzi wanaopokea milo katika siku za mafunzo ya mbali bado wanastahiki msaada wa P-EBT. Unaweza kupata milo hiyo na bado ukastahiki msaada huu.

Swali la 20: Nina watoto wengine ambao hawajaandikishwa shuleni. Je, wanastahiki msaada?

Jibu: Hapana. Msaada huu unapatikana tu kwa watoto ambao wameandikishwa katika shule ambayo kawaida hushiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana. Tafadhali angalia Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara kuhusu P-EBT kwa maelezo kuhusu watoto wanaostahiki msaada wa utunzaji watoto.

Swali la 21: Kadi ya P-EBT inaonekanaje?

Jibu. Hapa ni mfano wa sehemu ya mbele ya kadi.



P-EBT
Mmiliki wa kadi ya VT

Swali la 22: Kwa nini nilipokea barua yenye nambari ya huduma ya ustawi wa jamii ambayo sio yangu?

Jibu: Ikiwa ulipokea kadi ya P-EBT, ESD iliitengea “nambari bandia ya huduma ya ustawi wa jamii” kwa madhumuni ya kuamilisha kadi yako. Tafadhali tumia nambari ya huduma ya ustawi wa jamii iliyoorodheshwa kwenye barua (sio nambari yako halisi ya ustawi wa jamii) na ufuate maagizo haya ya kuamilisha kadi yako:

Jinsi ya Kuamilisha Kadi Yako:

1. Piga simu bila malipo 1-800-914-8605.
2. Tumia mfumo otomatiki ili kuchagua nambari ya siri yenye tarakimu nne.
3. Weka [INSERT FAKE SSN] unapoombwa kuweka nambari ya huduma ya Ustawi wa Jamii.
4. Unapoombwa kuweka tarehe ya kuzaliwa, tumia ile ya mtoto wako mkubwa iliyoorodheshwa kwenye barua uliyopokea.

Swali la 23: Watoto wangu hawakustahiki milo isiyolipiwa au iliyopunguzwa bei kabla ya COVID-19, lakini nimepoteza kazi yangu tangu wakati huo. Je, ninaweza kupata P-EBT?
Jibu: Ikiwa hali yako ya kifedha imebadilika, tunakuhimiza uombe:

- Misaada ya 3SquaresVT. Ikiwa unapata msaada wa kila mwezi, mtoto wako anastahiki milo isiyolipiwa shuleni na unaweza kupata msaada wa P-EBT.
- Milo isiyolipiwa au iliyopunguzwa bei kwa kuwasiliana na shule ya mtoto wako. Unaweza pia kupata fomu kwenye Tovuti ya AOE. Ikiwa kaya yako imepania kustahiki, utapokea msaada wa P-EBT kwa miezi ambayo mwanafunzi wako alikuwa akisoma kwa muundo mseto wa kujifunza au wa mbali. Maombi yaliyoidhinishwa yaliyowasilishwa kwa shule yako kabla ya tarehe 1 Aprili 2021 yanaweza kustahiki kupata msaada kuanzia Septemba 2020. Baada ya tarehe 1 Aprili, maombi yaliyoidhinishwa yatastahiki msaada kwa mwanafunzi tu katika mwezi wa sasa na miezi ya baadaye.

Swali la 24: Je, itakuwaje iwapo sitaki msaada huu?
Jibu: Ushiriki ni kwa hiari. Ikiwa utachagua kutoshiriki, aidha:

- Usitumie msaada wa ziada unaotolewa kwenye kadi yako ya EBT ya 3SquaresVT. *AU*
- Haribu kadi yako maalum ya P-EBT uliyopewa kwa kukata ukanda wa sumaku na kutupa kadi kwa njia salama. HURUHUSIWI kumpa mtu mwingine kadi yako.

Swali la 25: Je, msaada wa P-EBT una tarehe ya mwisho ya matumizi?
Jibu: Ndiyo. Msaada wa P-EBT utakwisha ikiwa kadi haitatumika ndani ya siku 274.

Swali la 26: Nina maswali zaidi. Ninaweza kupata maelezo zaidi wapi?
Jibu: Tembelea https://dcf.vermont.gov/esd/covid19/P-EBT au piga simu 1-800-479-6151 chagua 7 kwa maelezo zaidi. Tafadhali wasiliana na shule ya mwanafunzi wako ikiwa una

wasiwasi mahususi kuhusu ustahiki wa mwanafunzi wako kwa milo isiyolipiwa na iliyopunguzwa bei, au ungependa kubadilisha mkuu wa kaya au anwani ya barua ambayo itatumika kutoa kadi.

********** P-EBT ya Msimu wa Kiangazi**********

Swali la 27: P-EBT ya Msimu wa Kiangazi ni nini?
Jibu: Ni nyongeza ya msaada wa P-EBT kwa watoto wa shule wakati wa msimu wa kiangazi.

Swali la 28: Nani anastahiki msaada wa P-EBT ya Msimu wa Kiangazi?
Jibu: Kaya za Vermont zilizo na wanafunzi waliostahiki wakati wa mwaka wa masomo wa 2020-2021 na ambao waliandikishwa katika shule ya Vermont kabla ya Juni. Wanafunzi wanaostahiki ni wale ambao wanastahiki milo isiyolipiwa au iliyopunguzwa bei ama wanaohudhuria shule ambayo hutoa kifungua kinywa na chakula cha mchana kisicholipiwa kupitia Provision 2 au CEP.

Swali la 29. Ninawezaje kujua iwapo kaya yangu inastahiki?
Jibu: Shule ya mwanafunzi wako itaamua ikiwa mwanafunzi wako anastahiki, kulingana na vigezo vilivyotolewa na jimbo. Shule inaweza kuwasiliana nawe ili kuhakikisha kuwa wana taarifa sahihi kwenye faili. Tafadhali jibu ombi lao. Ikiwa unastahiki, utapata barua kutoka DCF inayoelezea jinsi na lini utapata msaada.

Swali la 30: Ikiwa tunastahiki, je, tutapokea vipi misaada hii?
Jibu: Ikiwa unapokea 3SquaresVT kupitia kadi ya EBT, utawekewa msaada wa P-EBT kwenye kadi hiyo. Ikiwa tayari umepokea kadi ya P-EBT mwaka wa 2021, utawekewa msaada wa P-EBT kwenye kadi hiyo. Ama sivyo, utapokea kadi maalum ya P-EBT. Tafadhali tunza kadi yako ya P-EBT.

Swali la 31: Nilipokea kadi ya P-EBT msimu uliopita wa kuchipua (2020), lakini sina tena. Je, hilo litakuwa tatizo?
Jibu: Hapana. Kadi mpya zinatolewa kwa mwaka 2021. Ikiwa utapata msaada wako kwenye kadi maalum ya P-EBT, tafadhali tunza kadi mpya unayopata. Msaada wa ziada unaweza kuongezwa kwenye kadi hiyo.

Swali la 32: Je, msaada wa Msimu wa Kiangazi unatolewa lini?

Jibu: Kuna duru mbili zinazotolewa za msaada wa P-EBT ya Msimu wa Kiangazi:

- Duru ya kwanza wa msaada wa P-EBT ya msimu wa kiangazi kwa wanafunzi ambao tayari wanastahiki milo isiyolipiwa/iliyopunguzwa bei au wanaohudhuria shule inayotumia CEP au Provision 2 hadi kufikia Juni inatarajiwa kutolewa mwezi Julai 2021.
- Kwa wanafunzi walioandikishwa katika shule za Vermont hadi kufikia Juni 2021, lakini wanaostahiki milo isiyolipiwa/iliyopunguzwa bei katika kipindi cha msimu wa kiangazi, msaada wao utatolewa mwezi Septemba 2021.

Swali la 33: Kipindi cha msimu wa kiangazi ni kipi kwa madhumuni ya kuomba milo isiyolipiwa/iliyopunguzwa bei na kupokea P-EBT ya Msimu wa Kiangazi?

Jibu: Familia ambazo bado hazistahiki milo isiyolipiwa/iliyopunguzwa bei zinaweza kutuma maombi wakati wowote hadi tarehe 16 Agosti 2021 na iwapo zitabainishwa kustahiki, zitapokea msaada kamili wa P-EBT ya msimu wa kiangazi. Familia zinazoomba milo isiyolipiwa/iliyopunguzwa bei baada ya shule kufungwa na mnamo au kabla ya tarehe 16 Agosti watapokea msaada wao P-EBT ya Msimu wa Kiangazi katika duru ya pili ya utoaji mwezi Septemba. Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ya milo isiyolipiwa/iliyopunguzwa bei kwa madhumuni ya kupokea P-EBT ya Msimu wa Kiangazi ni tarehe 16 Agosti 2021.

Swali la 34: Je, msaada wa P-EBT ya Msimu wa Kiangazi ni kiasi gani?

Jibu: Msaada wa P-EBT ya Msimu wa Kiangazi ni $375 kwa kila mtoto anayestahiki. Hiki ni kiasi cha msaada kinachotolewa sawia kwa wote cha wakati mmoja.

Swali la 35: Je, msaada wa P-EBT ya msimu wa kiangazi unalingana bila kujali idadi ya watoto katika kaya?

Jibu: Msaada wa P-EBT ya msimu wa kiangazi ni $375 kwa kila mtoto anayestahiki.

Swali la 36: Ikiwa ninachukua milo kwa mtoto wangu katika eneo la shule yetu ya *Kuchukua na Kuondoka* au ninatumia mipango mingine ya milo au vyakula, je, lazima nisitishe kufanya hivyo ikiwa nitapata msaada wa P-EBT ya Msimu wa Kiangazi? Je, itafanya tusistahiki msaada?

Jibu: Hapana. Bado unaweza kupata milo hiyo na ustahiki msaada huu.

Swali la 37: Nina watoto wengine ambao hawajaandikishwa shuleni. Je, wanastahiki msaada?

Jibu: Hapana. Tafadhali angalia Maswali Yanayoulizwa Sana kuhusu P-EBT ya Utunzaji wa Mtoto kwa maelezo kuhusu watoto wanaostahiki msaada wa P-EBT ya utunzaji wa watoto, ikiwa ni pamoja na msaada wa msimu wa kiangazi.

Swali la 38: Mtoto wangu alimaliza shule ya upili mwezi Juni 2021, je, mtoto wangu anastahiki?
Jibu: Ikiwa mtoto wako alistahiki milo isiyolipiwa/iliyopunguzwa bei mnamo Juni 2021, mtoto wako atastahiki msaada wa P-EBT wa msimu wa kiangazi.

Swali la 39: Mtoto wangu alimaliza shule ya upili mapema Januari 2021, je, mtoto wangu anastahiki?
Jibu: Hapana. Ili kustahiki P-EBT ya Msimu wa Kiangazi, mtoto lazima awe ameandikishwa shuleni ilipofika Juni 2021. Kwa kuwa mtoto wako alimaliza mnamo Januari, hawezi kufikiriwa kuwa ameandikishwa mwezi Juni.

Swali la 40: Je, mtoto wangu anapaswa kuhudhuria shule ya msimu wa kiangazi ili kustahiki P-EBT ya Msimu wa Kiangazi?
Jibu: Hapana. Kuhudhuria shule wakati wa msimu wa kiangazi sio kigezo cha kuamua ikiwa mtoto anastahiki P-EBT ya Msimu wa Kiangazi.

Swali la 41: Je, msaada wa P-EBT ya Msimu wa Kiangazi una tarehe ya mwisho ya matumizi?
Jibu: Ndiyo. Msaada wa P-EBT utakwisha ikiwa kadi haitatumika ndani ya siku 274.

Swali la 42: Mtoto wangu anastahiki milo isiyolipiwa na iliyopunguzwa bei alikuwa anasoma kwa muundo wa ana kwa ana katika mwaka wa masomo ya 2020-2021, je, mtoto wangu anastahiki msaada wa P-EBT ya msimu wa kiangazi?
Jibu: Ndiyo. Ustahiki unategemea ustahiki kwa milo isiyolipiwa/iliyopunguzwa bei.

Swali la 43: Nina maswali zaidi kuhusu msaada wa P-EBT ya Msimu wa Kiangazi. Ninaweza kupata maelezo zaidi wapi?
Jibu: Tembelea https://dcf.vermont.gov/esd/covid19/P-EBT au piga simu 1-800-479-6151 chagua 7 kwa maelezo zaidi. Tafadhali wasiliana na shule ya mwanafunzi wako ikiwa una wasiwasi mahususi kuhusu ustahiki wa mwanafunzi wako kwa milo isiyolipiwa na iliyopunguzwa bei, au ungependa kubadilisha mkuu wa kaya au anwani ya barua ambayo itatumika kutoa kadi.

VERMONT
AGENCY OF HUMAN SERVICES
DEPARTMENT FOR CHILDREN & FAMILIES

VERMONT
AGENCY OF EDUCATION